

HALMASHAURI YA MJI KASULU

(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi wa Mji)



Simu: +255282810335

Tovuti: www.kasulutc.go.tz

Baruapepe: td@kasulutc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi wa Mji
Halmashauri ya Mji Kasulu
S. L. P 475,
KASULU.

Unapojibu Tafadhali Taja:

KUMB NA.KSTC/I.2/9/92

15/06/2022

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.

Halmashauri ya Mji Kasulu imepokea kibali cha ajira kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Kufuatia kibali hicho Mkurugenzi wa Mji wa Kasulu anawatangazia watanzania wote wenye sifa na uwezo wa kutuma maombi ya nafasi hizo kwa kuzingatia sifa, vigezo na maelekezo yaliyo katika tangazo hili.

1. MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA LA II (NAFASI 3)

Sifa za Mwombaji

- Cheti cha Kidato cha IV au VI
- Aliyehitimu mafunzo ya cheti cha utunzaji kumbukumbu katika fani ya masijala

Kazi za Kufanya:-

1. Kutafuta kumbukumbu/ nyaraka/ mafaili yanayohitajiwa na wasomaji
2. Kudhibiti upokeaji, uandikishaji wa kumbukumbu/ nyaraka
3. Kuchambua, kuorodhesha na kupanga kumbukumbu/ nyaraka katika makundi kulingana na somo husika kwa ajili ya matumizi ya ofisi
4. Kuweka/ kupanga kumbukumbu/nyaraka katika reki katika masijala/ vyumba vya kuhifadhia kumbukumbu
5. Kuweka kumbukumbu (barua, nyaraka nk) katika mafaili
6. Kushughulikia maombi ya kumbukumbu/ nyaraka kutoka katika taasisi za serikali

MSHAHARA

Kwa kuzingatia ngazi ya Mshahara kwa watumishi wa Umma **TGS B₁** kwa mwezi

Masharti ya kazi

Kazi ina masharti ya kudumu na malipo ya uzeeni.

MAMBO YA KUZINGATIA KWA WAOMBAAJI

1. Muombaji awe raia wa Tanzania na awe tayari kufanya kazi sehemu yoyote katika Halmashauri ya Mji Kasulu
2. Awe mwenye umri kati ya miaka 18-45
3. Barua ya muombaji ziambatishwe na nakala za vyeti vya Elimu, Taaluma, cheti cha kuzaliwa na Picha mbili (2) za rangi (Passport size) za hivi karibuni
4. Barua za maombi ziambatishwe na maelezo binafsi ya muombaji (CV)
5. Testimonials, Provisional results, statements of results, hati za matokeo za kidato cha nne **HAVITAKUBALIWA**
6. Waombaji waliosoma nje ya nchi waambatishe uthibitisho wa vyeti vyao kutoka Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA)
7. Kila muombaji awe na kitambulisho au namba ya NIDA
8. Pia tangazo hili linapatikana kwenye tovuti ya Halmashauri ambayo ni;
www.kasulutc.go.tz
9. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **21/6/2022** saa **9:30 Alasiri**

Maombi yote yatumwe kwa Anwani ifuatayo;

Mkurugenzi wa Mji,
Halmashauri ya Mji,
S.L.P 475
KASULU.

Imetolewa na;



Dollar R. Kusenge
MKURUGENZI WA MJI
HALMASHAURI YA MJI KASULU



MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MJI
KASULU

Jiandae Kuhesabiwa Siku ya Jumanne Tarehe 23 Agosti, 2022